HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA

BARUA PEPE: mwalushusekondari@gmail.com
SIMU NA. 0621 94 33 74 Mkuu wa Shule
0629794083 Makamu Mkuu wa Shule

SHULE YA SEKONDARI MWALUSHU
S.L.P 166
BARIADI
TAREHE: .....

KWA .....
SHULE YA MSINGI .....
S.L.P 308
ITILIMA

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA SEKONDARI KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

1. UTANGULIZI

Nafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Mwalushu. **"HONGERA SANA"**

2. MAHALI SHULE ILIPO

Shule ipo kijiji cha **Mwamigagani** kata ya **Mwalushu**, tarafa ya **Itilima** wilaya ya **Itilima**

3. KUFUNGUA SHULE

Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021` na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021
Uchelewaji pasipo sababu za msingi hautavumiliwa na **SHERIA KALI** zitachukuliwa dhidi yako.

4. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

(A) SARE ZA SHULE

i. Wavulana

- Suruali mbili, moja **KAHAWIA** na nyingine **DARK BLUE** zenye **turn up** na marinda mawili kila upande. Tafadhali zingatia ni muhimu
- Shati mbili **nyeupe za tetron** mikono mifupi aina ya tomato
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba vinavyofunika miguu na vyenye visigino vifupi au flat
- Soksi **nyeusi** zisizo na alama yoyote ile. Tafadhali zingatia hili
- Viatu vya michezo
- Tai ndefu za rangi ya kahawia moja na dark blue moja (Ziendane na rangi ya suruali)
- Mkanda wa ngozi mweusi sio wa utambi
- Trakisuti na T-shirt za rangi ya nyekundu kwa ajili ya michezo

ii. Wasichana

- Sketi mbili, moja rangi ya **KAHAWIA** na na nyingine **DARK BLUE** mshono wa rindabox, kitambaa kiwe kizito sio mtumba, urefu unaoanzia juu kiunoni hadi kwenye kifundo cha mguu na isiwe na mpasuo
- Tai mbili aina ya Buterfly za rangi ya sketi
- Shati mbili **nyeupe za tetron** mikono mifupi aina ya tomato
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba vinavyofunika miguu na vyenye visigino vifupi au flat
- Soksi **nyeupe** zisizo na alama yoyote ile. Tafadhali zingatia hili
- Trakisuti na T-shirt za rangi ya nyekundu kwa ajili ya michezo

(B) VIPIMO VYA USHONAJI

Wavulana

- Suruali iwe na marinda 2 kila upande na ruksi 6
- Belt (Pindo) ya suruali nchi $1\frac{1}{2}$
- Paja nchi 23
- Chini nchi 18
- Mifuko 3
- Suruali iwe na turn up
- NB: Fundi anaposhona azingatie vipimo kwa kuzingatia umbo la mhusika mwenyewe

Ukurasa 1 kati ya 2

HEADMASTER
MWALUSHU SEC. SCHOOL
BOX 166 BARIADI

Wasichana

- Mshono wa rindabox
- Belt (Pindo) ya sketi nchi $1\frac{1}{2}$
- Sketi ifike kwenye kifundo cha mguu,
- NB: Sketi fupi hazitapokelewa

5. MAHITAJI MENGINE

- Mwanafunzi aje na daftari, counter book (quire 2) zisizopungua 9
- Begi zuri kwa ajili ya kubebea daftari (mifuko ya Bob haitakiwi)
- Kalamu za wino na risasi
- Mkebe wa hesabu (mathematical set)
- Aje na kamusi ya Kiingereza kwa Kiswahili
- Mwanafunzi awe na saa ya mkononi kwa ajili ya kutunza muda

6. MASOMO YAFUNDISHWAYO

- Masomo yanayofundishwa ni kumi (10) ambayo ni **Civics, History, Geography, Kiswahili, English language, Literature in English, Physics, Chemistry na Basic Mathematics.** Kwa kidato cha kwanza watakua na masomo tisa tu
- Masomo yote hufundishwa kwa lugha ya kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili
- Lugha ya mawasiliano shuleni ni Kiingereza

7. MENGINEYO

- Sheria, taratibu na kanuni (**STK**) za shule atazikuta shuleni mara baada ya kuripoti
- Mzazi/Mlezi pamoja na mwanafunzi mnatakiwa kusoma na kuelewa maagizo yaliyoelekezwa katika fomu hii na kuyafuata bila kuongeza wala kupunguza

8. MUHIMU

- Sare ambazo hazitazingatia vigezo/vipimo hazitaruhusiwa, hivyo mzazi/mlezi uwe makini katika ushonaji

9. KAULI MBIU YA SHULE

Kauli mbiu ya shule ni: **"ELIMU KWA AJILI YA KUJITEGEMEA"** (Education for Self Reliance)

10. MWISHO

Nakutakia maandalizi mema na hongera sana kwa kuchaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari katika shule ya sekondari Mwalushu. Karibu sana

MGABO MADUHU NGIDU
(MKUU WA SHULE)
10/12/2020
HEADMASTER
MWALUSHU SEC. SCHOOL
BOX 166 BARIADI

SHULE YA SEKONDARI MWALUSHU
SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE 2021

(A) SHERIA ZA SHULE

Mwanafunzi anatakiwa kuepuka makosa yafuatayo
Makosa haya yanaweza kusababisha afukuzwe shule kwa mujibu wa sheria ya wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia:

(i) Wizi wa aina yoyote
(ii) Ugomvi, lugha chafu, kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake au mtumishi
(iii) Udanganyifu katika mitihani ya aina yoyote
(iv) Kujaribu kusababisha na kuongoza ama kushiriki kugoma kwa mwanafunzi au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni
(v) Ubakaji , Ulawiti, Ushoga au Usagaji
(vi) Uasherati pamoja na kupatikana kuwa na vifaa vya aina hiyo
(vii) Ulevi wa aina yeyote
(viii) Uvutaji wa sigara, bangi na madawa ya kulevya pamoja na uuzaji
(ix) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule/umma na ya watu wengine
(x) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
(xi) Kutoa mimba, kushiriki au kushawishi kutoa mimba ndani na nje ya shule
(xii) Kukataa adhabu halali kwa makusudi
(xiii) Kudharau bendera na wimbo wa Taifa/Viongozi wa serikali, Picha za viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa
(xiv) Kuoa au kuolewa
(xv) Kutoonekana shuleni shuleni kwa muda wa siku 90 utafukuzwa na Bodi ya Shule

(B) KANUNI MUHIMU ZA SHULE

(i) Mwanafunzi anapaswa kuwa mtiifu, mwenye adabu na mnyenyekevu nyakati zote na popote. Zaidi ya yote awe na nidhamu ya hali ya juu
(ii) Mwanafunzi akiwa nje ya darasa asimame na kusalimia kwa heshima na adabu kwa walimu na wageni wote watakaotembelea shule
(iii) Marufuku kwa mwanafunzi kujiingiza katika mahusiano ya kimapenzi, wanafunzi wote ni watoto wa familia moja
(iv) Ni lazima kila mwanafunzi kuvaa sare sahihi za shule wakati wote na nyakati za shule
(v) Marufuku kwa wanafunzi kuonekana kwenye vilabu vya pombe, kumbi za sinema,kumbi za mpira na majumba ya kulala wageni pamoja na sehemu zenye michezo ya bahati nasibu
(vi) Ni marufuku kuvaa heleni,pete, kofia, kufuga nywele ndefu na ndevu, kusuka, kupaka rangi kucha na midomo pamoja na kutochomekea shati
(vii) Ni marufuku kuongea lugha zisizo rasmi shuleni mfano Kisukuma. Kiingereza ni lugha pekee ya mawasiliano
(viii) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi au laini ya simu shuleni na nje ya shule
(ix) Ni lazima kila mwanafunzi aoneshe bidii kubwa katika masomo darasani pamoja na mitihani ya mara kwa mara inayotolewa na walimu. Kutoonesha bidii kutasababisha upewe cheti cha **mwanafunzi dhaifu**
(x) Ni marufuku kuletwa au kuchukuliwa na usafiri wa gari, wala daladala za baiskeli na pikipiki hapa shuleni
(xi) Ni marufuku kuonekana mitaani mara baada ya saa 12:30 jioni, ukionekana hatua kali zitachukuliwa dhidi yako
(xii) Ni marufuku kutumia vipodozi, kubadilisha ngozi na kuweka nywele dawa
(xiii) Mwanafunzi anatakiwa kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
(xiv) Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
(xv) Mwanafunzi anatakiwa kutunza mali ya shule ama ya umma
(xvi) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
(xvii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
(xviii) Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea nyumba za walimu isipokuwa kwa kibali maalumu
(xix) Mwanafunzi unatakiwa uheshimu kengele
(xx) Kila mwanafunzi ahakikishe anazuia na kukamata mifugo inayoingia eneo la shule

Ukurasa wa 1 kati ya 1

HEADMASTER
MWALUSHU SEC. SCHOOL
BOX 166 BARIADI

Imesainiwa
MGABO M. NGIDU
10/12/2020